# SERA YA UREJELEZAJI WA TAKA NGUMU JIJINI DAR ES SALAAM

## Dibaji:

Mazingira safi kitovu cha afya bora na maendeleo kwa wananchi. Ili kufikia lengo la kuwa na mazingira safi, ni lazima kuwa na mikakati endelevu ya kudhibiti uchafuzi wa Jiji kutokana na taka ngumu zinazozalishwa kila siku.

Ili kuweka usimamizi endelevu wa usafi Jijini ni lazima kuweka misingi ya usimamizi, tathmini na kuchukua hadhari kuhusu madhara kwa mazingira, kwa kudhibiti taka kuanzia zinapozalishwa, ukusanyaji, usafirishaji na utupaji wake. Moja ya njia za kudhibiti taka ngumu ni kurejeleza taka kwa kuzifanya mali. Ili kupata matokeo mazuri ni lazima kuweka misingi ya utekelezaji ikiwa ni pamoja ushirikishwaji wa umma, utekelezaji wa sheria na makubaliano kwa wadau mbalimbali wanaojihusisha na sekta ama teknolojia ya urejelezaji taka.

Siku hizi katika nchi zote zilizoendelea imegundulika kuwa ni hatari na hasara kama taka zote zitatupwa mahali pamoja na kufunikwa tu bila kurejelezwa. Inaeleweka pia ya kwamba ndani ya taka kuna thamani kubwa kiuchumi. Kwa hiyo nchi nyingi duniani zimeanzisha taratibu za kutenganisha taka na kukukusanya kila aina ya taka peke yake.

Kwa mbinu ya kurejeleza tunaweza kuhifadhi mali asili na kutumia nishati kwa njia mwafaka zaidi. Pamoja na kulinda maliasili kurejeleza kwa taka pia huchangia katika kupunguza kiwango cha nishati kinachotumiwa katika mchakato wa kutengeza bidhaa viwandani. Faida nyingine ya kurejeleza ni kupunguza kiasi cha taka ngumu ambazo hukusanywa na kutupwa. Kwa njia hii, hupunguza uharibifu wa mazingira kupitia taka ngumu na pia kupunguza kiasi cha eneo la akiba linalohitajika kwa ajili ya kutupia taka.

Sipora J. Liana
**MKURUGENZI WA JIJI**
**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**

## Neno la utangulizi:

Jiji la Dar es Salaam linaundwa na Halmashauri 6 ambazo ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Halmashauri za Manispaa ya Ilala, Kinondoni, Temeke, Ubungo na Kigamboni. Halmashauri ya Jiji jukumu lake kuu ni kuratibu na kusimamia maeneo ya kutupa taka na kuelimisha jamii juu ya kuweka mazingira safi ikiwa ni pamoja na kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

Hali ya usafi wa Jiji la Dar es Salaam hususani udhibiti taka ngumu ni tatizo la muda mrefu ambalo lina changamoto nyingi. Tabia iliyozoeleka miongoni mwa jamii ya utupaji ovyo wa taka katika maeneo yasiyositahili imechangia Jiji kuwa chafu. Kuzagaa kwa taka kunaweza kuwa kichocheo cha milipuko ya magonjwa kama vile kipindupindu na magonjwa mengine ya kuhara na kutapika. Hali ya uchafu Jijini inachangiwa pia na elimu ndogo juu ya usafi wa mazingira, kutotii sheria zilizopo kwa upande wa wananchi na usimamizi hafifu wa sheria za usafi wa mazingira.

Ili kupunguza uchafuzi wa mazingira, Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam imeandaa sera ya urejelezaji wa taka ngumu ambayo itakuwa ni msingi muhimu kwa Taasisi za Serikali kuanza kutambua na kurasimisha sekta ya urejelezaji taka ambayo awali ilikuwa ikiendeshwa na Taasisi binafsi na vikundi visivyokuwa rasmi.

Urejelezaji wa taka una faida nyingi miongoni mwa jamii kama; kuongeza thamani ya taka na kipato katika jamii, kupunguza malundo ya taka katika mitaa na maeneo ya jamii, kupunguza gharama za uendeshaji wa dampo, kupunguza gharama za udhibiti taka katika Manispaa na kuongeza uelewa wa jamii katika uchambuzi wa taka kuanzia ngazi ya kaya.

Isaya Charles Mwita
**MSTAHIKI MEYA WA JIJI**
**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**

**DHAMIRA**

***Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam inakusudia kujenga Jiji lenye maendeleo endelevu yanayosimamiwa kwa kanuni ya utawala Bora ambapo wananchi hawaishi katika umasikini bali wanakuwa na kiwango kizuri cha maisha na Jiji lenye mazingira ya kiushindani yanayovutia wawekezaji***

**DHIMA**

***Kutumia rasilimali zote zilizopo ukiungwa mkono na ushiriki wa wadau, kutoa huduma bora na za uhakika kwa wote, Kupunguza umasikini na uchumi ukuao kwa kiwango cha juu na huduma zenye ubora wa juu zenye kuvutia na kuimarisha uwekezaji.***

## YALIYOMO


NENO LA UTANGULIZI............................................................ ii

DIBAJI............................................................................ iii

DHAMIRA........................................................................ iv

DHIMA............................................................................ iv

1.0 UTANGULIZI

1.1 Tafsiri..................................................................... 1

1.2 Taka zinazoweza kurejelezwa.................................... 1

1.3 Hatua muhimu za urejelezaji taka............................ 2

2.0 HALI YA TAKA NGUMU JIJINI......................................... 2

2.1 Uzalishaji............................................................ 2

2.2 Uhudumiaji wa taka............................................. 2

2.3 Urejelezaji wa taka.............................................. 3

2.4 Teknolojia ya urejelezaji taka nchini........................ 3

3.0 LENGO KUU.................................................................. 3

4.0 MALENGO MAHUSUSI.................................................. 4

5.0 USHIRIKISHWAJI......................................................... 4

6.0 HITIMISHO.................................................................. 5

# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Tafsiri

**Urejelezaji ni nini?**

**Urejelezaji** *(recycling)* ni mbinu ya kutibu taka kwa shabaha ya kuokoa malighafi zilizopo ndani ya taka na kuirejeleza kwa matumizi ya kiuchumi.

**Urejelezaji** taka ni tendo la uchakataji taka na kuziondoa katika hali ya uchakavu, ubovu au uharibifu na kuzirudisha katika hali ya ubora ili ziweze kutumika tena. Taka zilizorejelezwa zinafanyika malighafi kuzalisha bidhaa zingine kuzuia uzalishaji wa hewa ya ukaa ambayo ingesababishwa na utupaji wa taka husika.

**Urejelezaji** ni mbinu ya kutibu taka ambazo kwa kawaida haziwezi kutumika kupitia utaratibu wa kemikali au kusagwa kwa mashine. Baada ya kupitia utaratibu huu taka hizo hubadilishwa na kuwa katika hali ambayo inaweza kutumika kama malighafi ya kutengezea bidhaa nyingine.

Bidhaa nyingi tunazotumia hutengenezwa kwa kutumia malighafi inayotokana na vyanzo vya asili. Jinsi idadi ya watu inavyoendelea kuongezeka matumizi ya bidhaa mbalimbali pia yanaendelea kuongezeka. Jambo hili linapelekea kupungua na hata kumalizika kwa vyanzo vya asili. Ili kuweza kulinda vyanzo vya asili hatuna budi kuvumbua mbinu mpya na mwafaka wa kutengeneza bidhaa zinazohitajika. Miongoni mwa mbinu zilizovumbuliwa katika jitihada za kulinda vyanzo vya mali asili ni falsafa ya kurejeleza.

## 1.2 Taka zinazoweza kurejelezwa

Taka kama Chuma, shaba, risasi, karatasi, plastiki, aluminiam, mpira na kioo na nguo huweza kurejelezwa na kutumiwa tena kama malighafi kwa mara nyingine. Taka ya elektroniki na mafuta pia huweza kurejelezwa kwa urahisi. Kurejelezwa kwa taka husaidia katika kulinda rasilimali.

**1.3 Hatua muhimu katika urejelezaji**

Hatua ya kwanza katika utaratibu wa kurejeleza ni kutenganisha taka zinazoweza kurejelezwa kwa kuziwekwa katika sehemu tofauti na taka ambazo haziwezi kurejelezwa. Hatua hii ni muhimu sana katika mchakato wa kurejeleza na ni jambo muhimu sana kwa taka zinazoweza kurejelezwa kuwekwa katika pipa maalum.

**2.0 HALI YA TAKA NGUMU JIJI**

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inatambua ongezeko la aina tofauti za taka ngumu zikiwemo za taka za majumbani, taka za viwandani na taka za Hospitali ambazo hutupwa maeneo mbalimbali na hivyo kuweza kusababisha uchafuzi wa mazingira (hewa, maji na Ardhi).

**2.1 Uzalishaji**

Jiji la Dar es Salaam linakadiriwa kuzalisha zaidi ya tani 4,252 za taka kwa siku. Kati ya hizo ni asilimia 45 hadi 50 tu zinazopokelewa katika dampo sawa na tani 1,200 – 2,000 ya taka zinazokisiwa kuzalishwa kwa siku ambapo taka zinazobaki huishia kwenye maeneo ya wazi, mitaro ya maji, barabara na makazi.

**2.2 Uhudumiaji wa taka.**

Kama lilivyo jukumu lake la kisheria, Halmashauri ya Jiji inamiliki na kuhudumia dampo lenye ukubwa wa hekta 65 ambalo linaendeshwa kwa mtindo wa kupokea taka na kushindilia (controlled dumping) na si dampo la kitaalam (Sanitary landfill) hali ambayo imesababisha milima ya taka kiasi cha ujazo wa mita 2-3 katika eneo la karibu hekta 45. Hali hiyo imekuwa ikisababisha ugumu wa kupanga taka, kuzisukuma hasa kipindi cha mvua na kusababisha kukwama kwa magari, mitambo kufanya kazi kwa shida hivyo

kuhitaji matengenezo ya mara kwa mara pamoja na matumizi makubwa ya nishati ya mafuta.

### 2.3 Urejelezaji wa taka

Katika mataifa mengi yaliyoendelea na yanayoendelea, urejelezaji taka umekuwa ni njia mojawapo ya kudhibiti wingi wa taka zinazopelekwa dampo na umeweza kuongeza thamani ya taka. Njia hiyo imeweza kuhamasisha utenganishaji wa taka katika jamii kwani taka huwa mali ambayo watu binafsi na mwananchi mmoja moja hujiongezea kipato na kusaidia kusafisha mazingira kwa gharama nafuu. Maeneo ya viwanda na karakana za urejelezaji taka huweza pia kutengwa ndani ya maeneo ya dampo ili hupunguza shughuli za urejelezaji taka unaofanyika katika maeneo ya makazi.

### 2.4 Teknolojia ya urejelezaji taka nchini

Uchunguzi umeonyesha kuwa sekta ya urejelezaji taka bado haijatambuliwa na kurasimishwa katika mfumo wa Serikali. Kwa sasa kazi hizo zinafanywa na baadhi ya vikundi na makampuni binafsi (Informal sector) na wamekuwa wakifanya kazi hizo bila uratibu wa Taasisi yeyote ya Serikali aidha kwa kuwatambua wadau husika pamoja na maeneo wanayofanyia kazi za urejelezaji. Pia utafiti mdogo uliofanyika umeonesha kuwa masoko ya bidhaa za taka zinazorejelezwa zinapatikana nchini na nje ya nchi. Aidha inaonesha kuwa sekta ya urejelezaji wa taka ikisimamiwa na kuratibiwa vyema itaongeza ajira kwa vijana na jamii kuliko ilivyo sasa.

Urejerezaji wa taka ngumu unaweza kusaidia kuongeza viwanda vidogo vidogo, teknolojia mpya na kipato ambacho kimekuwa kikipotea ikiwa ni pamoja na kupunguza uchafuzi wa mazingira (hewa, maji na ardhi) hali ambayo huongeza hewa za ukaa na kuchangia mabadiliko ya tabia ya nchi.

## 3.0 LENGO KUU

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inalenga kuhakikisha kiwango cha juu cha uzuiaji wa uchafuzi wa mazingira kwa kuweka taratibu zitakazowezesha

aina nyingi za taka zinatakazozalishwa katika Jiji ziweze kurejelezwa (**Recycling and Re-use**) ili kuwa na Jiji safi.

## 4.0 MALENGO MAHUSUSI

Katika kuhakikisha hilo linafanyika Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam inalenga kufanya yafuatayo;

4.1 Kubuni miradi mbalimbali ndani ya Jiji itakayohusisha wadau mbalimbali inayolenga urejelezaji taka pamoja na masoko ya uhakika ya taka zilizorejelezwa au bidhaa zilizotokana na taka rejea.

4.2 Kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa kurejeleza taka ikiwa ni pamoja na kushirikiana na Halmashauri za Manispaa katika kuhakikisha utenganishaji wa taka unafanyika kuanzia ngazi za uzalishaji (sorting at source).

4.3 Kuwatambua na kuwaunganisha wadau mbalimbali wanaojihusisha na teknolojia za urejelezaji taka ndani ya Jiji la Dar es Salaam

4.4 Kutenga maeneo ya Viwanda vidogovidogo au karakana (**recycling facility**) ndani ya dampo au katika maeneo yake ambayo yatafaa kwa kazi zinazohusiana na urejelezaji taka.

4.5 Kuhamasisha teknolojia zinazolenga uzalishaji na utumiaji wa bidhaa zitokanazo na taka rejea.

4.6 Kuhakikisha inaweka mazingira bora yatakayowezesha ukuaji wa sekta ya urejelezaji taka ngumu kwa kuongeza viwanda na ubora wa bidhaa zake ili ziweze kupata soko ndani na nje ya nchi na hatimaye kukuza pato jamii na Taifa.

4.7 Kuwezesha wananchi wa maisha ya chini wakiwemo vijana na wanawake kushiriki katika ubunifu na utumiaji wa teknolojia za urejelezaji taka na hatimaye kuweza kuboresha usafi.

## 5.0 USHIRIKISHAJI

5.1 Halmashauri ya Jiji inategemea kuibua miradi inayohusiana na urejelezaji taka kwa kushirikiana na wadau mbalimbali vikiwemo

vikundi vya vijana na Wanawake ili waweze kushiriki kikamilifu katika sekta husika.

5.2 Halmashauri ya Jiji itashirikisha Manispaa ili ziweze kuzingatia na kuhamasisha jamii katika uwekaji wa miundombinu itakayosaidia utenganishaji taka (sorting) ili taka nyingi ziwe na ubora wa kurejelezwa.

5.3 Halmashauri ya Jiji itahamasisha makampuni binafsi kushiriki na kuongeza kiwango cha taka kitakachorejelezwa ndani ya jiji la Dar Es Salaam.

5.4 Halmashauri ya Jiji itazishirikisha Taasisi zinazojihusisha katika ubunifu wa teknolojia zinazoweza kutumika katika urejerezaji wa taka ili taka zote zitakazorejelezwa ziwe na ubora unaokubalika.

5.5 Halmashauri ya Jiji itatumia mikutano, vikao, makongamano na vyombo vya habari katika kuhamasisha urejelezaji wa taka na kutangaza masoko ya bidhaa husika.

5.6 Halmashauri kwa kushirikiana na Halmashauri zingine itahakikisha tathmini ya mara kwa mara inafanyika ili kugundua mafanikio na changamoto ili kuboresha sekta husika.

## 6.0 HITIMISHO

Sera ya Urejelezaji taka ngumu itasaidia kuwafanya wananchi waelewe kuwa taka ni mali, kuongeza wadau wa sekta ya urejelezaji, kukua kwa teknolojia, kuongezeka kwa ajira pamoja na upatikanaji wa bidhaa rahisi ikiwemo mifuko ya karatasi badala ya mifuko ya nailoni. Hali hii itapunguza taka zinazozagaa, kuchomwa na kusababisha uchafuzi wa mazingira unaosababisha mabadiliko ya tabia ya nchi. Kuongezeka kwa Urejelezaji pia kutasaidia kupunguza gharama za uzoaji taka katika Manispaa na gharama za uendeshaji wa madampo. Aidha sera ya urejelezaji itasaidia uhifadhi wa mazingira kwa kupunguza kiasi cha sumu zinazosambaa hewani, ardhini na katika maji na itapunguza gharama za vitu kwa kutunza thamani iliyobaki katika taka.